# *Kupanda Mzabibu Na Mahali Pa Kuupandia*

Tunayo mambo mengi sana, lakini Wewe unajua moyo wetu na unajua kila kitu tunachohitaji. Tuna furaha sana kwamba tunaweza kuyaleta Kwako katika maombi, tukijua ya kwamba Wewe unaelewa na utatupatia wema Wako; si kwamba tunastahili huo, bali kwa sababu Wewe umetuahidia huo. Nina hakika kwamba kuna haja nyingi kanisani asubuhi ya leo, kwa ajili ya ugonjwa na mhitaji. Nasi tungeyaleta Kwako kwa unyenyekevu sasa hivi, tukiomba rehema Yako njema na nguvu za uponyaji, kwa ajili ya kila mmoja wao.

2 Tunaomba pia kwa ajili ya ahueni na wale ambao hawangeweza kufika kanisani asubuhi ya leo. Pia, kwa wengi ambao wamekusanyika hapa sasa. Wengi ni wagonjwa na wahitaji. Tunawaona na magongo na wakiwa vitini, na viti vya magurudumu, nao wana—wanahitaji rehema Yako. Tunaomba, Bwana, ya kwamba utawajalia, kwa wingi. Jalia watoke hapa, wakishangilia, wameponywa na kupata afya. Wengi ambao hawaonyeshi mateso yao, lakini, hata hivyo, labda ugonjwa wa moyo uko karibu kuwachukua, ama kansa, ama pepo fulani anayeogopwa sana. Tunaomba, Bwana, ya kwamba atatupiliwa mbali asubuhi ya leo. Watatoka hapa, wenye furaha, wazima.

3 Tungemkumbuka maskini mvulana yule a—anayekufa. Ndio kwanza tuambiwe, na mpendwa, kwamba ana kansa na atakufa leo hii, kama rehema Yako haitatandazwa kwa mtoto huyo. Ee Bwana Mungu, umrehemu maskini mvulana huyo. Mpe ukombozi, Bwana; yakiwa ni mapenzi Yako ya Kiungu. Tuna furaha sana kwa ajili ya ushuhuda wake, ya kwamba ameikubali Damu Yako, sana hata amemwomba baba yake kumzika kwa rangi nyekundu, wapate kujua ya kwamba alikuwa amefunikwa na Damu. Tunakushukuru Wewe, Bwana, kwa maskini imani hodari kama hiyo ya mashujaa wadogo, wanapopiga hatua kwenda kukabiliana na mwisho wa maisha, wakiukumbatia msalaba mioyoni mwao, na hapo kuonyesha alama ya Damu. Ikiwezekana, Bwana, mwokoe maskini mvulana huyo mdogo, mjalie aishi. Tumewaombea wengine.

4 Halafu basi, Bwana, tunaziombea ibada asubuhi ya leo. Kuna wengine hapa, labda, ambao hawakujui Wewe kama Mwokozi wao. Ikiwa ndivyo ilivyo, jalia hii iwe ndiyo siku ambayo watakuona Wewe kuwa wa thamani maishani mwao, kama Mwokozi. Wale wanaohitaji uponyaji, wakupate kama Mponyaji. Bwana, naomba uje kwa mtumishi Wako, asubuhi ya

leo. Naomba nikupate kama Mhubiri. Kwa kuwa, tunalikabidhi hili Kwako, tukiomba ya kwamba Wewe utajibu katika Jina la Bwana Yesu. Amina.

5 Sikuzote tunafurahia kuja katika nyumba ya Bwana, na kwenye Kusanyiko la Mzaliwa wa kwanza. Nami nilikuwa, kama kawaida, nimechelewa. Sikuwazia nitafika hapa, isipokuwa niombe lifti. Huu ni utani mzuri kwa mke wangu. Ameketi humu ndani, mahali fulani. Aliondoka asubuhi ya leo, nami nilikuwa chini kwenye orofa ya chini nikisoma. Ndipo yeye akasema, "Ninazo funguo, Billy." Na kumbe, alikuwa na funguo za gereji, pia. Nisingeweza kuingia. Nilikuwa na wakati mbaya sana.

6 Ndipo baada ya kitambo kidogo, Billy akanikosa, naye akasema, "Sijui ni kwa nini hajaja." Ndipo akaniita.

7 Nikasema, "Njoo upesi sana." Nikasema, "Kwa sababu sina njia ya kushuka kwenda kanisani." Kwa hiyo sisi ni . . . Nina furaha kuwa hapa. Kwa hiyo, nimechelewa.

8 Lakini, mwajua, tunapokaribia ule ulimwengu mwingine, ambapo wakati hautakuwako tena, tunaanza kusahau kuhusu wakati. Yote yanaingiana na Umilele, wala hapatakuwapo na wakati tena. Hakuna kipimo cha wakati.

9 Hapana shaka Paulo alikuwa na kitu kama hicho niani mwake, ule usiku alipohubiri usiku kucha. Mvulana mmoja alianguka kutoka kwenye jengo hilo akafa. Ndipo Paulo akaulaza mwili wake juu ya huyo mvulana, nao uhai ukamrudia tena huyu mvulana.

10 Ninaamini niliambiwa, na mchungaji, sasa hivi, ya kwamba wana mtoto mchanga wanayetaka awekwe wakfu asubuhi ya leo. Kwa hiyo kama huyo mama atamleta huyo jamaa mdogo, sasa hivi, tutamkabidhi kwa Bwana, yeye ama mama, yeyote yule. Na kidogo ninapenda ibada za kuwekwa wakfu. Waweza kuja mbele, Ndugu Neville?

11 Habari za asubuhi, dada. Jina la jamaa huyu mdogo ni nani? [Dada huyo anasema, "Frank Wayne Dabney."—Mh.] Frank Wayne Dabney. Wewe si wa mbari ya Robert Dabney, sivyo? Frank Wayne Dabney, yuna umri gani? ["Majuma manane."] Majuma manane. Hajawa katika ulimwengu huu katili muda mrefu sana. Vema, yeye ni tunda la ndoa yenu. Na sasa mnataka kumkabidhi kwa Mungu, apate kuwa mtumishi Wake. Hiyo ni kweli, dada? Mungu awabariki.

12 Vema, ninashika hazina moja ndogo hapa, mrembo sana. Hebu mwangalieni tu, mtoto Frank Dabney.

Na tuombe.

13 Mpendwa Baba wa Mbinguni, katika siku za kutembea Kwako hapa duniani, katika umbo la mtu, aitwaye Bwana Yesu, walikuletea watoto wadogo. Ndipo ukawawekea mikono Yako na kuwabariki, na kusema, "Acheni watoto wadogo waje

Kwangu, wala msiwakataze, kwa kuwa walio kama hao Ufalme ni wao." Mama huyu anamkabidhi mikononi mwangu, asubuhi ya leo, maskini mvulana huyu, ambaye namkabidhi Kwako. Ninaomba, Bwana, ya kwamba Wewe utambariki huyu jamaa mdogo. Bariki nyumba yake. Jalia alelewe katika nyumba ya Kikristo. Katika maonyo ya Mungu, jalia alelewe. Na kukiwako na kesho, jalia aihubiri Injili kama imekusudiwa hivyo na Wewe. Mpe maisha marefu, ya afya. Wabariki wazazi wake. Jalia kila jambo jema uliloahidi, limjie mvulana huyu mdogo. Mama amemkabidhi mikononi mwetu, kama wazee wa kanisa. Na sasa tunamkabidhi Kwako. Katika Jina lake Yesu Kristo, naomba umbariki mtoto huyu. Amina.

Mungu akubariki, mtoto Frank. Nafikiri wanapendeza sana!

14 Nilipaswa kuwaombea wakati nikiwa na upako...?... Tunazo leso hapa za kuombewa, lakini afadhali nifanye hivyo tukianza kuwaombea wagonjwa, na upako kwa ajili ya ibada uje. Ndipo tungekuwa bora zaidi kama tungaliwaombea wakati huo.

15 Nafurahi kuwaona wengi wa marafiki zangu humu ndani. Ninaamini ninamwona Ndugu Charlie Cox kule nyuma mkutanoni. Na pia ninamwona Ndugu John O'Bannon, kutoka Louisville. Na marafiki wengine wengi, huku, ambao na— nawatambua. Na kwa hiyo tuna furaha sana kuwa nanyi humu, mkikusanyika pamoja nasi asubuhi ya leo, kumtumikia Bwana.

16 Sasa tunatarajia, baada ya kitambo kidogo, kuanzisha uamsho hapa kwa siku chache. Tunaombea jambo hili. Ninajisikia ya kwamba Mungu asipouleta uamsho, ama kuuweka moyoni mwetu, basi huo uamsho ni juhudi zetu wenyewe. Halafu basi tukingojea, Naye ajisikie kwamba ni wakati wa uamsho, kisha alitie hilo moyoni mwetu, basi tutajisikia kuwa na uamsho.

17 Rafiki mwingine anayeketi hapa, baba na mama ya Ndugu Wood na mmoja wa wadhamini wetu hapa kanisani. Tuna furaha kuwa nao asubuhi ya leo.

18 Nami nikishuka mtaani, jana, jamaa mmoja aliyeishi hapa mjini, ambaye alikuwa maskini jamaa mkali sana. Nami sikuzote nilimpenda, na ni mvulana mzuri. Naye mke wangu alikuwa ni jirani yao. Na kidogo alikuwa ni mwimbaji, na mwanamuziki. Naye alikuwa akiketi kule na kuupigapiga mguu wake, huku amevaa kofia kubwa ya kaoboi, na fidla msumeno. Lakini alifanya kazi kwenye WPA. Basi siku moja jambo fulani likatukia, ambalo sikuzote lilinikumbusha, ama nililiweka niani mwangu, hasa, kwa muda mrefu. Kamwe halikuniacha. Alikuwa na watoto wadogo kadha; mke mzuri. Walikuwa maskini hohehahe, kama sisi sote tulivyo.

19 Basi nikamwona, amesimama kwenye kipandio, mstarini, akingojea cheki hiyo ya WPA ije. Mtu wa posta akaja mtaani.

Walikuwa na furaha sana. Kesho yake ilikuwa ni Pasaka. Walikuwa wakienda kununua peremende za Pasaka au kitu fulani, wakati cheki ya baba itakapoingia. Basi mtu wa posta alipokuja, hakuwa na cheki ya baba. Unaona huo mtazamo wa masikitiko kwenye nyuso za hao jamaa wadogo, nalo sikuzote limekaa nami, masikitiko makubwa sana.

20 Sikumwona huyo mtu, kwa miaka kadhaa. Ndipo jana, nikishuka mtaani, wakati mimi . . . Mimi na mke wangu tulikuwa tukitoka kwenye supamaketi, ama Quaker Maid katikati ya mji, tulikutana na nani, uso kwa uso, ila yeye? Basi moja ya mambo ya kwanza waliyotaka kuniambia, alikuwa amekuwa Mkristo. Hakuwa amekunywa pombe kwa miaka kadhaa. Nami nina furaha kuwa pamoja nawe, Bw. Logston, unayeketi kwenye kiti cha mbele, hapa kanisani, asubuhi ya leo. Yeye ni mshiriki wa kanisa la Ndugu Junior Cash huko Charlestown, Indiana, ndugu mzuri sana. Ni vema zaidi kuwa Mkristo kuliko ilivyo huko nje ulimwenguni. Sivyo? Sasa, nafikiri yeye huimba kwenye vile vipindi, na kucheza muziki wake, kwa utukufu wa Bwana. Kumbukumbu nyingine tu ya neema ya ajabu ya Mungu.

21 Ungetaka kusimama, Bw. Logston? Sininii . . . Mtu huyu wakati mmoja alikuwa mlevi. Mmoja wa hawa hapa wacheza dansi motomoto, mwajua, fidla na kadhalika. Sasa yote yamebadilishwa yakawa kwa Ufalme wa Mungu, naye yuko hapa nje, akisema, "Asante, kwa ajili yake, Bwana." Loo, wakati . . .

22 Nilikuwa nikimwambia Bw. Wood, jana. Nikasema, "Wakati wewe na mama, mtakapofika upande ule mwingine na kupata jumba lenu kuu, basi asubuhi moja wakati mmefurahi sana, na huko chini kabisa ng'ambo ya vilima, na kushuka bondeni, mahali fulani, ambapo kuna kibanda kidogo kilichojengwa mle. Nitakapotembea barazani, na kufika hapo na kusimama barazani, nitarudisha mwangwi kote kwenye mabonde hayo:

> Neema ya ajabu! jinsi hiyo sauti ilivyo tamu,
> Iliyomwokoa mwovu kama mimi!
> Wakati mmoja nilikuwa nimepotea, na sasa nimepatikana,
> Nilikuwa kipofu, lakini sasa naona.

23 Nilimwambia Bw. Wood, nikasema, "Vema, mguse mama begani, useme, 'Mungu asifiwe! Maskini Ndugu Branham alifaulu. Yule pale, huko chini katika kibanda chake kidogo.'" Kama kamwe nikifika Kule, itakuwa ni kwa neema ya ajabu ya Bwana Yesu.

24 Sasa tunaweza kuinamisha vichwa vyetu kwa muda kidogo tu kabla hatujalifungua Neno.

25 Bwana sisi ni kitu kama kundi la watoto. Tuna vipengele vyetu vya kibinadamu, pia, sisi, ucheshi wetu, ushirika wetu pamoja. Sasa tunaifikia sehemu ile takatifu sana ya

ibada, kulisoma Neno lisiloweza kukosea la Mungu aliye hai. Ningeomba, Bwana, ya kwamba utanena kwa kila Neno. Jalia litoke na kuzama mioyoni mwa watu, na litapata mavuno yaliyotarajiwa. Jalia Roho Mtakatifu mkuu aje miongoni mwetu sasa, na kuyachukua Maneno haya yatakayosomwa, na kutugawia, kila mmoja, kama tunavyohitaji. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu na kwa ajili Yake. Amina.

26 Katika Zaburi ya 80, ninataka kusoma shehemu moja.

> *Wewe uchungaye Israeli, usikie, wewe umwongozaye Yusufu kama kundi; wewe. . .uketiye katikati ya makerubi, utoe nuru.*
>
> *Mbele ya Efraimu . . .Benyamini na Manase, uziamshe nguvu zako, uje, utuokoe.*
>
> *Ee Mungu, uturudishe,. . .uangazishe uso wako; nasi tutaokoka.*
>
> *Ee* B*WANA*, *Mungu wa majeshi, hata lini utayaghadhibikia* maombi *ya watu wako?*
>
> *Umewalisha mkate wa machozi; umewanywesha machozi kwa kipimo kikuu.*
>
> *Unatufanya sababu ya ugomvi kwa* jirani *yetu; na adui zetu wanacheka wao kwa wao.*
>
> *Ee Mungu wa majeshi, uturudishe,. . .uangazishe uso wako; nasi tutaokoka.*
>
> *Ulileta mzabibu kutoka Misri, ukawafukuza mataifa, ukaupanda.*

27 Somo langu asubuhi ya leo, Bwana akiliruhusu, kwa muda mfupi tu, litakuwa: *Kupanda Mzabibu Na Mahali Pa Kuupandia*.

28 Ni ajabu jinsi ambavyo Mungu, mahali pengi, huwawakilisha watu Wake katika njia mbalimbali. Si muda mrefu uliopita tulikuwa tukizungumzia mahali ambapo Yeye alituwakilisha kama tai, na Yeye akiwa ndiye Tai Mwenyewe, nasi tai Wake wadogo. Nami ninatumaini ya kwamba kila kitu kitaendelea vizuri. Mara ya mwisho nilipolizugumzia hilo, nilipata barua ambapo. . .Ule mji mkuu, wengi wenu mnajua mahali ulipokuwa, huko Ohio, ambako shirika la wahudumu lilikusanyika pamoja na kuzihukumu ibada zangu kwa sababu kuwa ninaamini kwamba Mungu alimwitia mtu Uzima wa Milele kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Na kwa imani yangu, endapo Mungu ni Mungu, alipata kuwa Mungu, Yeye angali ni Mungu, na sikuzote alikuwa ni Mungu. Iwapo hakunijua kabla ulimwengu haujakuwapo, basi Yeye si Mungu.

29 Wengi wenu mmekuwa mkisoma hapa kwenye uwanja wa maonyesho, na kadhalika, juu ya upambanuzi huu unaozidi hisia

ya kawaida. Na baadhi ya huo, hakika, umeenda upogo kwa huduma yangu. Lakini, kama ulipata kusoma ama ulikuwa na njia yoyote ya kusoma mitholojia, kisasili: "kitu kinachoonekana kana kwamba ndicho, bali sicho."

30 Na katika Maandiko, tunaona ya kwamba Yambre na Yane walishindana na Musa kwa kufanya jambo lile lile hasa walilofanya, kwa kutupa fimbo chini nayo ikageuka kuwa nyoka. Musa aliagiza mapigo. Nao wangeweza kuagiza mapigo, pia, bali wasingeweza kuyaondoa hayo mapigo. Wasingeweza kuponya, kwa sababu Mungu ndiye mponyaji pekee. Lakini wangeweza kuleta mapigo, ndipo Musa akayaondoa. Ndipo shindano la mwisho likaja, ambapo Musa alifanya kama vile tu Mungu alivyomwambia kufanya.

31 Nami ninajua, haya yote yanayoendelea, ulimwenguni siku hizi, hatimaye yatafikia kwenye shindano moja kubwa la kuamua siku moja. Maana, Biblia ilisema, "Kama vile Yane na Yambre walivyoshindana na Musa, ndivyo watu walioharibikiwa na akili, kuhusu Imani, watakavyoshindana katika siku za mwisho, lakini upumbavu wao utadhihirishwa." Ni unabii ambao hauna budi kutimizwa, nanyi mnaweza kuona pande zote mbili zikiinuka sasa.

32 Lakini Musa alifanya vile hasa Mungu alivyomwambia afanye. Alitupa chini fimbo nayo ikageuka ikawa nyoka. Nao hawa waaguzi wakatoka na kuzitupa chini fimbo zao nazo zikageuka kuwa nyoka. Musa alifikia mwisho wa akili yake, na mwisho wa nguvu zake.

33 Lakini hapo ndipo Mungu anapotaka kutufikisha, kufikia tu mwisho wa safari yetu, ndipo Yeye anaingia. Ni kama Yeye tu. Labda wewe ni mgonjwa sana, asubuhi ya leo, mpaka daktari anasema huwezi kuishi. Mtu anayezama atashikilia unyasi. Hivyo ndivyo ilivyo wakati tunapojaribu kufikia . . . Yote tunayoweza kufanya, sisi wenyewe, ambayo ni ya kibinadamu, hayo tutayafanya. Bali inapofikia mahali ambapo hamna tumaini lingine, hao wasioamini katika uponyaji wa Kiungu wataamini mara moja basi. Ndilo tumaini lao pekee.

34 Basi Musa alikuwa kwenye mwisho wa safari yake, ndipo Mungu akaingia na kumfanya huyo nyoka kuwala hao nyoka wa huyo mtu mwingine. Ndipo nyoka wake hakuwako tena.

35 Sasa, katika upambanuzi unaozidi hisia za kawaida, na katika mitholojia, na wote wanaowasiliana na mizimu. Hebu mimi, kabla tu sijaanza kwenye somo langu, niwaweke sawa kabisa kwa jambo hili, kwa msaada wa Mungu, nikiweza. Ibilisi anaweza kuyafanya mambo yaonekane sawa, bali sikuzote yanathibitika kwamba si sawa. Sasa, kamwe hawajaweza kufanya picha ya moja ya roho hizi hapa walizo nazo itokee, kwa sababu kweli haziko.

36 Lakini inapofikia wakati wa Mungu kuithibitishia sayansi, Yeye alikuwa ni Mungu, Yeye aliruhusu ile picha ipigwe. Inadumu milele. Mchunguzi alisema, "Nuru iligusa lenzi. Ile Nuru kweli ilikuwako. Haikuwa ni saikolojia." Kwa hiyo, mnaona, yale Mungu afanyayo yanadumu.

37 Nyoka wa Musa aliwameza nyoka wa hao wengine. Naye angeweza kuiokota kwa mkono wake, nao nyoka wao walikuwa ndani ya fimbo hiyo. Yale ibilisi afanyayo ni hadithi ya uongo. Yale Mungu afanyayo ni halisi. Kwa hiyo, ninapenda hili lizame ndani kabisa mioyoni. Mungu anapomwokoa mtu, yeye ameokoka. Usiwe na wasiwasi juu ya kurudi nyuma kamwe; huwezi. Kile Mungu afanyacho ni cha Milele. Ibilisi anaweza kukuchochea na kukufanya uamini umeokoka. Lakini wakati Mungu anapokuokoa kweli, unao milele, kwa sababu unao Uzima wa Milele. Yesu alisema hivyo.

38 "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka yuna Uzima wa Milele, wala hataingia hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Huo ni wa Milele kama Mungu Mwenyewe alivyo, kwa sababu ni Neno Lake.

39 Mungu ni Mungu mmoja. Yeye hawezi kujichanganya na mambo mengine, Yeye hagawanyiki. Mungu ni Mungu. Amri ya kwanza, ni, "Usiwe na miungu wengine mbele Zangu."

40 Kwa hiyo huwezi kuchanganya mafuta na maji na kuyafanya yafanye kazi vizuri. Yanapaswa kuwa ama ni maji au mafuta. Naye Mungu angali ni Mungu yeye yule. Tunayo dini inayochanganya mambo na kusema, "Mungu alikuwako, wakati mmoja alifanya *hivi*, wala hafanyi hivyo siku hizi," basi tunajaribu kuchanganya mafuta na maji. Kwa sababu, Yeye . . .

41 Maandiko yalisema, "Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele." Kamwe halitachanganyana na kutokuamini; imani haitachanganyana nako.

42 Tunamwamini Mungu. Ni ya Milele. Kutokuamini sikuzote kumekuwako, tangu bustani ya Edeni. Mungu sikuzote amewataka watu Wake kuamini jambo hili. Amewataka kuwa na imani, na ku—kujionyesha Mwenyewe miongoni mwa watu Wake. Mungu ni Roho.

43 Katika Yohana Mtakatifu mlango wa 15, kifungu cha kwanza, Yesu alisema, "Mimi ndimi Mzabibu; ninyi ni matawi." Sasa, tawi na Mzabibu vimeunganishwa pamoja. Naye Mungu daima amejaribu kuwapata watu ambao angeweza kuishi ndani yao, hata angeweza kuonyesha utukufu Wake miongoni mwa watu Wake.

44 Kwa hiyo tunasoma hapa ya kwamba Daudi alilia, na kusema, "Ee Bwana Mungu, uturudie tena. Tumetenda dhambi na kuondoka Kwako. Wewe unayekaa katikati ya madhabahu na kerubi, utuangazie tena." Kwa kuwa yeye alijua ya kwamba wakati mmoja Yeye alikuwa ni Mungu miongoni mwao, naye

Daudi alijua ya kwamba Yeye alikuwa angali ni Mungu. Watu walikuwa wamejitenganisha na Yeye. Mungu hakuangaza tena. Si kwamba asingeweza kuangaza. Ni kwa sababu watu walizizima rehema Zake kwao, kwa dhambi yao. Ndipo Daudi analiendea somo letu. Zaburi 80:7.

45 Akasema, "Uling'oa mzabibu, kutoka Misri, na ukauleta na kuupanda mahali pazuri." Hao walikuwa ni Waisraeli, watu wa Mungu waliokuwa huko Misri. Walikuwa mzabibu mzuri. Walikuwa wateule wa Mungu. Lakini kama mzabibu mzuri haujapandwa kwenye ardhi nzuri, hautazaa matunda mazuri. Inategemea huo mzabibu umepandwa wapi, itaamua matokeo ya hilo zao. Kwa hiyo, Mungu aliwahamisha Israeli, kutoka kwenye nchi kame.

46 Ni kitu kama siku hizi. Tunao, nchini, waaminio wengi mashuhuri na wazuri, nao wamechanganyikana katika makanisa yote ya kimadhehebu. Wanatoka katika madhehebu mbalimbali na matabaka mbalimbali ya maisha. Hiyo ndiyo sababu, katika huduma yangu, sijawahi kujaribu, wakati wowote, kumdhalilisha mtu yeyote yule wala dhehebu lolote lile, kwa sababu, katika hayo yote, kuna watu wema. Hao ni watu walioitwa na kuchaguliwa na Mungu.

47 Wewe ungaliweza kuwahukumu Israeli walipokuwa Misri? Walishika tu njia mbaya. Nazo dhambi zao zilikuwa zimewatenganisha na—na Mungu, nao wakapandwa huko Misri.

48 Hivyo ndivyo watu wengi walivyo, makanisani siku hizi, watu wazuri tu waliopandwa mahali pabaya. Sasa kama mwaminio halisi akiletwa kwa Kristo, naye amepandwa katika dhehebu kubwa ambalo haliamini katika miujiza na ishara na maajabu ya Bwana, mtu huyo huenda akawa ni Mkristo halisi, na Mkatoliki, Mbaptisti, Mpresbiteri, Shahidi wa Yehova, kitu kingine. Katika kanisa hilo, Mzabibu halisi wa Mungu, lakini kanuni ya imani ya kimadhehebu huukatilia mbali Uhai wa Mzabibu huo. Hauwezi kuzaa matunda Yake.

49 Na, kwa kawaida, matunda unayopata kutoka kwenye mzabibu uliodumaa ama usio kwenye ardhi nzuri ni matunda mabaya. Yatatokea kama matofaa, nayo yajae vifundo na kuliwa na wadudu. Yanakuwa ya kuliwa na wadudu wote.

50 Mzabibu mzuri wenye afya hata sio lazima unyunyiziwe. Una afya ya kutosha kuwatupilia mbali adui zake wote.

51 Ndivyo ilivyo na Mkristo aliyezaliwa mara ya pili. Haikupasi kuwa ukiwanyunyizia wakati wote, na kuwapapasa mgongoni. Hao wana afya ya kutosha kiroho kutupilia mbali kashfa yote ya ulimwengu. Wanaishi kwa mlo wa kweli.

52 Mti wakati mwingine, ambao. . . ama mmea ambao umekuwa mahali pa jangwa, na hauna unyevu wa kutosha kuulisha, utazaa maskini tunda dogo lililojaa vifundo, wala

halionekani kama tunda linalopaswa kutoka kwenye mzabibu wake.

53 Ndugu yangu, dada, hivyo ndivyo ilivyo na makanisa siku hizi. Mwenye dhambi huingia, baadaye, labda, wakati wa kuja nyumbani chini ya ushawishi, anaenda na kuisoma Biblia yake, kisha anaenda kanisani. Badala ya kupata matofaa makubwa matamu sana ama zabibu, Maisha ya Bwana Yesu yakionekana tena Kanisani, anapata maskini mawazo duni ya kimadhehebu, yaliyojaa vifundo, yaliyoliwa na wadudu. “Sisi Wabaptisti, tunalo. *Hao* hawana uhusiano wowote nalo. Sisi Wamethodisti, tunalo.” Mikono ya Mungu inafika kutoka bahari hata bahari, na kutoka pwani hata pwani, inaweza kuokoa hata wa mwisho. Lakini hayo ndiyo tunayopata katika mahali tunapoenda.

54 Ni kama vile Daudi pia alivyosema, tena, katika Zaburi 1. Yeye alisema, “Heri mtu yule asiyeungana na hawa wenye kudhihaki na wasio watawa, wasioungana nao, wasioketi pamoja nao. Mnajua, wenye kudhihaki wanaosema, ‘Siku za miujiza zimepita. Na ubatizo wa Roho Mtakatifu ni kujisingizia tu imani.’ Heri mtu ambaye hatafanya hivyo. Heri mtu yule atakayesimama mbali na jambo kama hilo. Hawataki kuchanganya hayo pamoja. Wala huwezi kuyachanganya mambo hayo pamoja. Heri mtu yule ambaye hatajiunga na moja ya mambo hayo yanayozikana Nguvu za Bwana.”

55 Biblia ilisema, “Tokeni miongoni mwa watu kama hao, kwa kuwa siku yaja ambapo watakuwa wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu; wenye mfano wa utauwa, bali wakikana Nguvu zake: hao nao mjiepushe nao.”

56 “Heri mtu yule asiyeketi na hawa wenye dhihaka, wanaofanya mizaha, wanaoliita Kanisa la kweli, ‘kundi la walokole.’ Atakuwa kama mti uliopandwa kandokando ya mito ya maji.” Mungu amemweka mahali maalum. “Tunda lake halitanyauka. Atazaa majani yake na matunda kwa majira yake.” Angalia jinsi Daudi alivyoyaandika hayo. “Mtu huyu amebarikiwa. Atapandwa,” sio tu kuwekwa. Mnajua, ninapenda kuona chochote kilichopandwa.

57 Sasa, Israeli, huko Misri, hawakuwa wamepandwa. Walikuwa wamewekwa tu. Haikuwa nchi yao ya asili. Naye mtu aliye Mkristo, anayeweka kikomo chake cha Milele juu ya kanuni fulani ya imani ya kimadhehebu, yeye hayuko katika mahali pake pafaapo. Alizaliwa apate kuwa huru, na mwana wa Mungu, kumwabudu Mungu. Lakini yeye yuko chini ya kanuni ya imani, hawezi kuzaa tunda lake, hata hivyo kitu fulani ndani yake kinatamani kufanya hivyo.

58 “Atakuwa kama mti uliopandwa kando ya mito ya maji.” Mito, wingi; maji, umoja. Mito mingi ikiingia katika mkondo huo mmoja. Kwa maneno mengine, atakuwa kama mtu katika Maandiko, ambaye anaamini Neno lote la Mungu, ambapo zile

Nguvu na zile karama tisa za kiroho zinaweza kutiririkia, kupitia kwa Mungu mmoja, kuingia ndani ya utu wake wa ndani kabisa.

59 Watu hawaamini katika kupiga makelele. Jambo ni kwamba, hawana furaha ya kiroho. Na furaha za maji ya Uzima zinaweza kutiririka. Hiyo kwa jumla ndiyo shida ya Maskani ya Branham, kwa sababu kwamba kutokuamini, masumbuko ya ulimwengu yalikuwa yamewafunga watu mpaka hawawezi kukua kiroho.

60 Hiyo ndiyo shida ya taifa letu. Hiyo ndiyo shida ya makanisa yetu. Hayana furaha. Nayo furaha ya Bwana imetoweka. Kama ilivyoandikwa wakati mmoja katika Maandiko, lile neno la Kiebrania la Ikabodi, linalomaanisha, "Uwepo wa Bwana umeondoka." Hiyo iko juu ya makanisa yetu, kwa sababu kwamba tuliuacha ule msingi wa asili, na kujiweka katika kanuni za imani na madhehebu, na kuruhusu mambo ya ulimwengu kuukausha ujuzi wetu pamoja na Mungu.

61 Loo, nenda pamoja nami hadi Arizona. Hebu nikupeleke katika majangwa, ambamo nilizunguka-zunguka kwa miaka mingi sana. Kila kitu jangwani kina mwiba juu yake. Kila mmea mdogo unaoufikia, usiukaribie, utakuchoma. Daima miiba yake imetokeza moja kwa moja, tayari kuchoma kitu chochote kinachoukaribia. Kuna shida gani? Ni kitu gani kilichoufanya mwiba? Ni kwa sababu haukuwa na maji. Hiyo ndiyo iliyoukausha. Mwiba huo ni jani, lililojikunja. Kwa sababu ya ukosefu wa maji, linakuwa mwiba.

62 Ndivyo ilivyo na Kanisa, siku hizi, hapo kanisa linapoondoka kwenye ile Chemchemi ya Uzima. Linapoondoka kwenye furaha za wokovu, linapomwacha Bwana Mungu, basi mtu huyo anakuwa mwiba, sikuzote anatafuta makosa, akichoma-choma. Mara unapotokea, "Mimi ni Mpresbiteri. Mimi ni Mmethodisti. Mimi ni *hiki-na-hiki*. Usinizungumzie juu ya upuuzi huo." Mwiba! Hauna matunda.

63 Ukiuchukua mmea uo huo, mpungate, kisha uuweke ardhini kwa vizazi vichache, ambako kuna maji mengi, basi mwiba huo utajifungua na utakuwa jani laini, linalozaa tunda.

64 Shida ya kanisa ni nini siku hizi? Limewekwa katika dhehebu, ambalo limeweka kanuni za imani za kimadhehebu na kulifunga, hakuna furaha, nyunyizo moja tu mara kwa mara, ya maskini uamsho mdogo wa kulishikilia. Linalohitajika kuwa, ni kutoka miongoni mwa wenye kudhihaki na wasioamini, na kupandwa kandokando ya mito ya maji.

> Kwa kuwa kuna Chemchemi iliyojaa Damu,
> Iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli,
> Ambapo wenye dhambi, (wasioamini) wakitumbukia chini ya hayo mafuriko,
> Hupoteza waa lao lote la hatia.

65 "Mti," Daudi alisema, "uliopandwa kandokando ya mito ya maji." Loo! Mungu Mwenyewe hawezi kutiririkia kwenye mpungate.

66 Sasa, maji yanawakilisha uzima. Tunajua ya kwamba Musa, huko nyikani, yeye aliupiga ule Mwamba, nao ukatoa maji ya uzima kwa watu waliokuwa wakiangamia. Naye Yesu alisema, "Kama vile Musa alivyoupiga ule mwamba nyikani, ndivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa juu," Naye alipigwa.

67 Uhai uko kwenye seli ya damu. Wala Uhai huo hauwezi kutoka mpaka seli hiyo ya Damu imekatizwa na kuvunjwa.

68 Wakati Mungu alipowatoa Israeli nje, Yeye aliwapa jaribio, kama taifa. Aliwang'oa huko Misri, miongoni mwa wasioamini. Na kuwaleta katika uangalizi Wake mwema, juu ya mbawa za tai, yule tai mkubwa, Musa, aliyewaongoza mahali mahali, akijaribu kuwaandaa, wapate kuvuka. Kwa muda wa miaka arobaini Yeye aliwaongoza na kuwalisha nyikani. Naye akailisha ardhi, ardhi nzuri, ardhi maalum. Naye akaonyesha mwujiza Wake, ishara na maajabu, kwa muda wa miaka arobaini nyikani. Alitoa miujiza na ishara, kwa nabii huyu, kuonyesha kwamba Yeye alikuwa ni Mungu. Ni nani angaliweza kuikausha bahari ila Yeye? Ni nani angaliweza kuipiga Misri ila Yeye? Ni nani aliyethubutu kuinua mkono ila Yeye? Lakini, katikati ya hayo yote, Yeye alikuwa ni Mungu, Naye alijionyesha Mwenyewe kuwa ni Mungu. Hakika aliwataka watu Wake kufanya hivyo.

69 Ndipo akailowesha ardhi ya Palestina, kwa damu ya mbuzi na ndama, mafahali, kondoo. Lakini hao watu wasingeweza kusimama. Haikutosha, kwa sababu uhai wa huyo fahali . . . Seli ya damu ilivunjika, nao uhai wa huyo mnyama ukarudi, usingeweza kupatana na uhai wa mwanadamu.

70 Siku moja, Mungu alidhamiria ya kwamba angewaokoa watu Wake, Kanisa Lake lililokusudiwa tangu zamani. Ilimbidi kufanya hivyo, Mwenyewe, kwa sababu alilichagua kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.

71 Mwanadamu ni mshindwa, na sikuzote atakuwa ni mshindwa. Yeye ameshindwa, kwanza kabisa, na daima atakuwa mshindwa.

72 Mungu, katika kuchagua Kwake tangu zamani, katika nia Yake kuu isiyo na kikomo, alipanga mpango wa kuweka chini Mzabibu halisi. Naye akapanda juu ya dunia hii, Mzabibu, Mzabibu wenye haki; sio dhehebu, sio kanisa, sio kanuni ya imani, bali Mtu, Mwenyewe, aliyefanyika mwili. Naye akadhihirisha amani Yake, Nguvu Zake, yule Malaika mkuu wa Mungu. Yehova mkuu alikuwa pamoja Naye. Na ndani Yake mlikaa utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili. Wala watu hawakumwamini; nao hawakumwamini kwa sababu asingeshirikiana na kanuni yao ya imani.

73 Hatimaye, walimwongoza hata Kalvari. Hapo hiyo seli ya Damu ikavunjwa, ya Mwana wa thamani wa Mungu, Mwili ambamo Yehova aliishi. Kulitokea Mzabibu, wenye mizizi Yake Utukufuni, matawi Yake yakiwa duniani, kuzalisha Kanisa la Mungu aliye hai, ambalo lingeonyesha kufufuka Kwake na Nguvu Zake. Ni akina nani hawa wanaume na wanawake ambao wangelikana Kanisa hilo, Mzabibu wa Mungu aliye hai? Kule kushindwa daima . . . Uwepo wa Bwana Yesu pamoja na Kanisa Lake, kuishi, na kuonyesha matawi Yake yaliyochaguliwa tangu zamani, aliyoyashika kabla ya kuwekwa misingi ya dunia. Na kuapa, kwa hao, ya kwamba Yeye angewafufua. Nalo Kanisa Lake, siku hizi, pamoja na utukufu wa kufufuka Kwake ukiishi ndani Yake! "Mimi ndimi Mzabibu; ninyi ni matawi." Kila wakati moyo unapopiga, damu hupigapiga kwenye kila kiungo cha mwili. Kila wakati moyo mwaminifu wa Mungu unapopiga, unapigapiga kupitia kwa Jina la Yesu Kristo, kwa Kanisa, "Lolote mtakaloomba kwa Jina Langu, hilo nitalifanya. Niko pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari."

74 Si ajabu Petro alisema, kwenye Siku ya Pentekoste, "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtajazwa na Uzima kutoka kwenye ule Mzabibu." Roho Mtakatifu akitoa Jina Lake, kwamba, kama tumeunganishwa pamoja Naye. Yeye ameunganishwa na Mungu, kwa sababu Yeye alikuwa Shina na Mzao wa Mungu.

75 Alikuja duniani. "Dunia iliumbwa na Yeye. Alikuja ulimwenguni; wala ulimwengu haukumtambua."

76 Na sasa, siku hizi, Yeye, baada ya kufa Kwake, kutoa seli ya Damu, ivunjike, ili kwamba kupitia kwa Damu ya Yesu Kristo Kanisa liweze kutakaswa na kuwekwa katika utaratibu. Ili kwamba, yule Roho Mtakatifu mkuu, ambaye ndiye Uzima wa huo Mzabibu, Uzima wa Milele wa ule Mzabibu, huyo Roho Mtakatifu aweze kupigapiga katika kila mshirika wa Kanisa la Mungu aliye hai.

77 Si ajabu hao ni watu wa ajabu na wa kipekee. Si ajabu wanatenda kigeni. Hawana tena shughuli za ulimwengu huu, kwa kuwa wamekufa na kuzikwa katika Kristo, nao wamefufuka kwa maisha mapya, wapate kuwa malimbuko ya wale wanaoufurahia ufufuo wa kiroho, kwamba Roho Mtakatifu angepitia kwa kila mshirika, na kuonyesha utukufu wa Mungu, kama ule Mungu aliouonyesha Misri wakati alipouleta ule Mzabibu.

78 Sasa, kunao mzabibu mwitu. Biblia inanena habari Zake katika Wafalme wa Pili. Na je, mliona, wakati mhubiri huyu alipotoka kwenda kuchuma njegere, alizitoa kwenye mzabibu mwitu. Mizabibu hiyo mwitu haina budi kukulia karibu na seminari mahali fulani, maana ilikuwa kwenye shule ya manabii.

Basi akachuma mkono mmoja wa matango-mwitu. Akayatupa kwenye birika, na kujaribu kuyachanganya na mboga halisi, za kweli. Nao wakalia, "Kuna mauti kwenye chungu."

79 Ndugu, kuna mzabibu mwitu unaokua, nao unakua kando ya kanuni ya imani, dhehebu. Ndipo unapofika kule nje, unakatiza furaha yote ya kiroho. Ndipo muda si muda wajua, mzabibu huo umekufa.

80 Lakini Mungu ameyakinia ya kwamba mzabibu Wake hautakufa. Kwa hiyo akaung'oa, kutoka kwenye kanuni hizo za imani, na kuujaza na Roho Mtakatifu, na kuuweka chini, katika Jina la Yesu Kristo. Humo Kanisa hilo linaweza kupigapiga na kuishi, na kufurahia, kuuhisi Uwepo wa Mungu aliye hai, likimwangalia Yeye akitenda kazi na kufanya mambo aliyofanya alipokuwa hapa duniani.

81 Kwa nini? Matawi Yake, uhusiano Wake, shina Lake, mwanzo Wake, ulikuwa ni Mungu. Alikuwa Mwana-Kondoo aliyechinjwa kabla ya kuwekwa msingi wa ulimwengu. Kabla hapajakuwapo na ulimwengu, Yeye alikuwa pamoja na Mungu. Alikuwa ndiye Shina na Mzao wa Daudi, Nyota ya Asubuhi, Ua la Bondeni. Huyo alikuwa Ndiye.

82 Mizizi Yake imezungushiwa Mungu, kukizunguka Kiti cha Enzi, kuuzunguka Ufalme wa Mungu. Mizizi Yake imezungushiwa. Uhai Wake umeenea hata duniani. Naye aliutoa Uhai Wake, ili aweze kurudi kwenye mizizi na kupigapiga tena, apate kuzaa matawi kutoka kwenye Mzabibu huo, ambao ni Kanisa Lake likionyesha matokeo yale yale aliyofanya wakati alipokuwa hapa duniani, kumfanya yule yule jana, leo, na hata milele.

83 Ee enyi Kanisa la Mungu aliye hai, aminini huu, Ukweli! Huyo hapo. Wakati Roho wa kweli wa Mungu anapotenda kazi juu ya mwaminio, lolote Maandiko yasemalo, atasema, "Amina." Mbona? Roho Mtakatifu ndiye aliyeiandika Biblia, yuko ndani yake, akiyapigapiga maisha yake. Yeye hajali ni nani anayeketi karibu, ama yale mtu mwingine yeyote asemayo. Sikuzote litaendana na Neno.

84 Kuna ya uongo. Ni matango. Yametoka kwenye mzabibu mwitu. Ni mzabibu mkubwa, unaifunika dunia nzima, bali ni mauti. Mengi ya hayo yametupwa miongoni mwa watu.

85 Lakini, kumbukeni, "Unga" unayapa Uzima tena, unayang'oa na kuyaweka mahali pazuri, ambapo ni Kristo Yesu. Chochote Neno Lake lilicho, na liwe "amina," kwako. Ndipo Roho wa Mungu, basi, furaha ya kiroho itatiririka kama mto. "Atakuwa kama mtu, mti, uliopandwa kando ya mito ya maji. Majani yake hayatanyauka. Hataketi kwenye kiti cha wenye mizaha ama cha asiyeamini, ama mtu mwovu anayeishi kwa kufuata mambo ya ulimwengu, bali atazaa matunda katika majira yake." Ni tunda la aina gani? Kama umepandwa katika

Kristo, utazaa matunda ya kiroho, matunda ya kiroho ya Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu anaishi ndani yako.

86 Yalinenwa vema, na yule mwanamke kisimani. Katika kufunga, tungesema hivi. Yeye alisema, hapo alipomwona, alionekana kama mtu wa kawaida. Hapakuwapo na lolote la kuvuti-ana sana juu Yake, la kuvutia, hasa.

87 Kwa kuwa Maandiko yalisema, "Hana uzuri hata tumtamani. Tulimficha nyuso zetu."

88 Nao wanafanya jambo lile lile siku hizi. Iwapo hawastawi kutokana na matunda ya kiroho ya Roho, kama hawastawi juu ya mambo yanayomhusu Mungu, Kristo ni kitu chenye sura mbaya kwao, "Kundi la watakatifu wanaojibingirisha, kundi la wendawazimu ambao wameharibikiwa na akili."

89 Lakini, kwa mwaminio, yeye analikumbatia. Ni Uzima wa Milele. Hakuna kinachoweza kututenganisha na upendo wa Mungu. Wala mauti, wala huzuni, wala njaa, wala chochote kinachoweza kututenganisha. Sisi tuko salama Milele katika magango Yake. Haya basi, hapo anapoukumbatia msalaba huo.

90 Yule mwanamke alisema, wakati. . . Yeye aliuliza swali, "Waweza kunipa maji ninywe?"

91 Mwanamke akasema, "Lakini sio kawaida Kwako, mwanamume, Myahudi, kumwuliza Msamaria, mimi mwenyewe, swali kama hilo."

92 Akasema, "Lakini kama ungalijua. . ." Kwa maneno mengine, namna hii, "Kama ungalijua jinsi ulivyokuwa karibu na ile Chemchemi ya Uzima, ningalikupa maji ambapo hutakuja hapa kuchota. Nitakupanda kwingine, wewe Msamaria. Nitakuleta, wewe mwenye dhambi." Huyo ni asiyeamini, wala haliamini. "Iwapo tu utaniacha Mimi nikung'oe asubuhi ya leo, Yeye alisema, nitakupanda kandokando ya mito ya maji. Nitakuweka mahali fulani, kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, ambapo utaamini kila Neno ninalosema ni Kweli. Utaniacha tu nikung'oe, asubuhi ya leo, ungekuwa tawi zuri. Wewe si wa shamba hilo la mizabibu mwitu. Wewe ni wa *hapa*, kwa hiyo hebu nikung'oe; nikupande katika Jina Langu, kandokando ya mito, kila kijito cha Neno la Mungu. Kwa kuwa kila Neno la Mungu ni la kweli. Kila ahadi ya Kiungu ni Kweli. Nitakupanda kandokando ya mito ya maji mamoja, Mungu mmoja. Nawe utazaa tunda, katika majira yako. Matawi yako hayatanyauka. Na lolote ufanyalo litafanikiwa. Utasimama wakati hakuna mahali pengine pa kusimamia. Utasimama, kwa vyovyote vile, ukijua ya kwamba Mungu alifanya hiyo ahadi. Hebu nikung'oe," Yeye alisema, "na kukupanda huku kandokando ya Maji haya, hata i—isikulazimu kukimbilia mahali hapa pa kanuni za imani, na mahali pa madhehebu, kutafuta. Huwezi kulipata kule, kwa vyovyote vile. Hebu nikung'oe, kandokando ya kisima hiki cha kale hapa kilichokauka, hata inakulazimu kuchukua

ndoo za mabati, na kuchacharisha na kuzozana, na kunywa kidogo, na kurudi na kunywa kidogo. Nitakupa Uzima wa Milele, furaha, kama tu kisima, kinachobubujika hadi Uzima wa milele. Niruhusu. Acha nikufanyie hilo," Kristo alimwambia yule mwanamke, mwenye dhambi.

93 Naye anasema jambo lile lile kwa Kanisa asubuhi ya leo. Mnajua Mungu yupo. Mnaamini Mungu yupo. Lakini katika ushirikishwaji wenu, kitu fulani kiliwakatilia mbali. Mko jangwani. Hakuna furaha ya kiroho. Mngetaka kujisikia kama walivyojisikia kwenye Siku ya Pentekoste. Hivi hamngependa kuwa na furaha waliyokuwa nayo?

94 Wakati Mungu alipomimina Uzima Wake, ndani ya tawi la kwanza la huo mti, mti huo ulianza kutenda kama walevi. Waliyumbayumba chini ya nguvu za Roho. Maskini wanawake watakatifu wapendwa kama bikira Mariamu, huko nje wakitenda kama walevi. Loo, alilewa kwa Roho. Naye akajaribu kuzungumza, wala asingeweza. Alikuwa na *kigugumizi*, ambacho kinamaanisha "kugawanyika," ni kugugumiza, kujaribu kusema kitu. Alikuwa amejaa sana Roho, asingeweza kulisema. "Uh-uh-uh-uh," midomo ya kugugumiza. Halafu, ghafla, kwa lugha nyingine, walinena.

95 Basi maskini mhubiri ambaye hakujua vya kutosha kuandika jina lake mwenyewe kwenye kipande cha karatasi, alipindua sanduku la sabuni ama chochote kile, ama kisiki, akakirukia.

96 Vema, hao wasioamini wakaanza kusema, "Watu hawa wamelewa. Hao ni lile kundi la watakatifu wanaojibingirisha."

97 Maskini jamaa huyu akayachukua Maandiko; sio kitabu cha kanuni za imani, bali Maandiko. Kasema, "Enyi watu wa Israeli, nanyi mkaao katika Yerusalemu, jambo hili na lijulikane kwenu. Kwa kuwa hawa hawajalewa kama mnavyodhania, kwa kuwa ni saa tatu mchana. Lakini hili ni *lile* lililonenwa na nabii Yoeli, 'Itakuwa katika siku za mwisho, asema Mungu, nitaimwaga Roho Yangu,' hiyo ndiyo inayowapigapiga."

98 Je, ungetaka kung'olewa kutoka kwa kanuni ya kale ya imani ya namna fulani, na kuwekwa kandokando ya Chemchemi ya Uzima, ambapo ni amani kama mto?

99 Mauti, yenyewe, kwa mvulana mdogo aliyesimama kule, amejaa kansa, bali amempokea Roho Mtakatifu. Nao madaktari wanamwambia yuafa. Baba yake alimwuliza, "U—unaogopa?"

100 Akasema, "Niko tayari. Niko tayari. Na ili kuuachia ulimwengu huu ushuhuda, nizikeni katika rangi nyekundu, kwa kuwa itakuwa ni ishara ya kwamba Damu ya Yesu Kristo imenifunika."

101 Hivyo ndivyo inavyofanya. Furaha, kama mto, unaweza kutembea mbele ya mauti, utembee mbele ya ulimwengu,

utembee mbele ya majaribu, usimame mbele ya wakosoaji na kunawiri kama Malaika. Kwa nini? Maisha yako si yako mwenyewe. Umekufa, nawe umezikwa katika Jina la Yesu Kristo, na kufufuka tena kwa Maisha mapya. Yeye anaweza kupigapiga kupitia kwako, baraka Zake, na kuzaa matawi yaliyounganishwa na ule Mzabibu. "Nitaiweka mahali maalum." Mungu alisema Mwanawe alikuwa ndiye chaguo Lake.

102 Unaingiaje katika Kristo? Petro alisema nini kwenye Siku ya Pentekoste, jinsi ya kuingia katika Kristo? Alisema, "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo, kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa hao walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie." Huo ulikujumuisha wewe, huo wito. "Tubuni, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu. Ahadi hii ni kwa ajili yenu."

103 Loo, ndugu, Roho wa kweli wa Mungu atapigapiga kwenye Hilo, aseme, "Hiyo ni Kweli." Yaangalie hayo matango na mzabibu mwitu. Lakini Roho wa kweli wa Mungu, anayetaka kupandwa mahali maalum, ambapo matunda ya Roho.

104 Naye Yesu alifanya nini basi? Alisema, "Kwa kuwa mwanamke huyo anataka kukubali hayo . . . "

Alisema, "Bwana, nipe Maji hayo. Ninataka Maji hayo."

105 Kasema, "Acha maskini mtungi wako wa kale ukae hapo. Huhitaji mtungi wa maji wa namna hiyo tena. Huhitaji barua yako kwa kanuni yako ya imani. Achana na njia zako za kujiita Presbiteri, Baptisti, Methodisti, Pentekoste, ziweke nyuma. Njoo kwenye Chemchemi hapa. Nami nitakujaza sana kwa furaha itakayotiririka kama mto."

106 Kama vile yule maskini mtu mweusi alivyosema, "Nina amani kama mto." Inatiririka usiku na mchana. Mbele ya mauti, inatiririka vivyo hivyo.

107 Paulo alisema, "Ewe mauti u wapi mwiba wako? Nawe kaburi u wapi ushindi wako? Lakini Mungu ashukuriwe atupaye ushindi kupitia Yesu Kristo." Bila shaka.

108 Akamwangalia. Akaanza kuzungumza Naye kuhusu mahali pa kuabudia. Naye akamwambia, "Nenda kamwite mumeo." ("Nitamwacha ajue kama Mungu angali hai. Mimi Ndimi Mzabibu.") "Nenda kamwite mumeo."

"Mbona," akasema, "Sina mume."

109 Akasema, "Hiyo ni kweli. Umekuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako."

110 Akageuka. Ilikuwa ni kitu gani? Ku—kupandikizwa kwake, uhai wa maisha yake, ambapo alikuwa ameng'olewa kwenye mti huu wa kale wa kanuni ya imani, palikuwa pameshika,

wakati kupigapiga kwa kwanza kwa Mungu kulipoingia kwenye matawi yake.

111 "Bwana, naona ya kwamba Wewe ni nabii. Nami ninajua Maandiko yalisema ya kwamba Masihi atakuja Naye atafanya jambo hili."

Akasema, "Mimi Ndiye. Mimi Ndiye."

112 Aliacha kanuni hiyo ya kale ya imani ikae pale. Upesi tu alivyoweza kukimbia, akaanza kuitangaza hiyo habari. "Njoni, Mwone Mtu Ambaye aliniambia mambo niliyofanya. Haimkini Huyu kuwa ndiye Masihi? Masihi ni Mungu aliyetiwa mafuta. Alimtambua Yeye kama Mungu, nabii Imanueli, Mungu.

"Mimi ni Mzabibu. Ninyi ni matawi."

113 Akasema, "Vema, ninyi watu, ninyi Wayahudi huabudia Yerusalemu. Mnalo kanisa kubwa huko juu, na kanuni ya imani."

Akasema, "Ninajua hilo."

Mwanamke akasema, "Tunaabudu katika mlima huu hapa."

114 Akasema, "Ninajua hilo. Lakini wakati unakuja, na sasa upo, wakati kanuni hizo za imani za Yerusalemu, ama kanuni hii ya imani ya Kisamaria, haitafanya kazi. Kwa kuwa Mungu ni Roho, nao wanaomwabudu hawana budi kumwabudu katika Roho na katika Kweli."

115 Hilo ndilo tawi linaloishikilia ile Kweli. "Tubuni, kila mmoja wenu mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi yenu," nanyi mtaunganishwa pamoja na lile tawi. Mtakuwa na haya, jambo lile lile, kwa kuwa Roho wa Mungu atapigapiga kupitia kwenu, awaletee, mito ya furaha, amani, subira, imani, wema, upole, unyenyekevu. Atakupa, kukufanya utoke kwenye. . .Kutoka mbwa mwitu, atakufanya mwanakondoo. Kutoka kwa mwewe, atakufanya hua. Unaona? Ni Roho wa Mungu aliye hai ambaye anabadilisha asili yako. Sasa njoni Kwake, mkapandikizwe na kuwa mmoja wa matawi Yake. Kwa kuwa siku moja . . .

116 Hiyo Kamba okozi iliyokuwa imewekwa hivi, ni Uhai wa Kristo, Roho Mtakatifu, iliyounganishwa na Ufalme wa Mungu. Mungu atashukia kwenye hilo tawi la Milele, siku moja, nao wote hao waliokufa katika Kristo Yeye atawaleta pamoja Naye, wakati akiinua ule Mti tena. Uliopandwa kandokando ya mito ya Uzima, ambapo Mti usiokauka kamwe haunyauki wala kupoteza majani Yake.

117 Wakati ukikukabidhi tawi asubuhi ya leo, rafiki yangu mpendwa, lipokee, kisha ung'olewe kutoka dhambini mwako, ung'olewe kutoka kwenye mashaka yako, kutoka kwenye kanuni yako ya imani.

118 Sikwambii uliache kanisa lako. Wewe kaa na kanisa lako, bali umjie Kristo. Jambo ndilo hilo. Sijali unaenda kwenye kanisa gani, maadamu umekuja kwenye Chemchemi hiyo iliyojaa Damu.

119 Upokee Uzima Wake, na uuache ukuinue, ukuinue kutoka kwa kuvutiwa na ulimwengu, mpaka mambo yote ya ulimwengu yamekufa. "Yeye aipendaye dunia, au mambo ya dunia, kumpenda Mungu hata hakumo ndani yake." Huwezi kuweka uhai wa mboga ndani ya mzabibu, kisha uzae zabibu. Unaona? Endapo wewe ni wa Kristo, unayapenda mambo ya Kristo. Umejazwa na Roho. Wewe ni . . . Yeye ndiye Mzabibu; ninyi ni matawi. Hebu akupokee asubuhi ya leo, kama alivyompokea yule mwanamke Msamaria, na kuuweka uhai wako ndani ya Uhai Wake, na kukufanya kiumbe kipya.

Wakati tukiviinamisha vichwa vyetu kwa muda kidogo tu.

120 Kabla ya maombi, kunaweza kuwa na wengine ambao wangeinua mkono wao, waseme, "Niombee, ndugu. Ninataka kuunganishwa sana katika Kristo." Mungu aubariki moyo wako. Loo, hilo ni zuri sana. "Ninataka kuunganishwa sana, katika Kristo, hata maisha yangu yatanawiri kwa ajili Yake. Niondoe kwenye (jamani) woga wangu wote, na mashaka, na maudhi, na kanuni za imani. Na unipande ndani Yake, asubuhi ya leo, ambapo ninaweza kuwa na amani kama mto. Nina wasiwasi sana. Sijui ninaelekea wapi. Sijui jinsi ninavyoweza kusimama. Niweke hapo."

121 Sasa wakati tumeviinamisha vichwa vyetu, ninyi mwezao, mlioinua mikono yenu, je, mnaweza kusimama kwa miguu yenu, kwa maombi mafupi tu? Ninii tu . . . Tutawaombea, papo hapo mlipo. Maana, tuna ninii . . . Simameni moja kwa moja kwa miguu yenu sasa, tupate kuomba.

122 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . kuwaondolea, fadhaa zote. [Sehemu tupu kwenye kanda.] . . . kushirikiana na waovu wake; mkatembee katika Nuru mpya, tangu leo na kuendelea. Lijalie, Bwana.

123 Wewe umesema, "Ombeni, nanyi mtapokea. Tafuteni, nanyi mtapata. Bisheni, nanyi mtafunguliwa." Sasa wanabisha. Ninaomba. Jalia wapokee, Bwana. Jalia siku hii iyabadilishe maisha yao hivi kwamba, kamwe hapatakuwapo na shaka nyingine niani mwao. Na jalia waje Nyumbani Kwako, kwenye Siku ile.

124 Wamesimama, Bwana, asubuhi ya leo. Wamesimama kwa ajili Yako sasa, mbele ya wanadamu wenzao. Wewe umesema, "Yeye atakayefanya jambo kama hilo, nitamtetea mbele za Mungu na Malaika watakatifu. Lakini kama akinionea aibu, basi, kwenye Siku hiyo, nitamwonea aibu." Bwana, hawaoni aibu, asubuhi ya leo. Wamesimama. Sasa, Wewe hulitimiza Neno Lako. Wajaze kwa Roho Wako, na uwape maisha ya utumishi,

ili kwamba, katika ulimwengu ujao, waweze kufurahia ule Uwepo usioshindwa wa Bwana Yesu. Tangu leo, na kuendelea, tunawakabidhi Kwako, katika Jina la Yesu. Amina.

125 Mungu awabariki. Mtu fulani karibu nao awape mkono, aliye karibu nao.

Kuna Chemchemi . . .

126 Sasa ujumbe umekwisha, sasa mwabuduni Bwana, kwa njia fulani fungeni tu macho yenu.

. . . Damu,
Iliyotolewa kwenye ninii ya Imanueli . . . (Huyo alikuwa ni Mungu, Imanueli.)
Nao wenye dhambi, (wasioamini) wanapotumbukia . . .

Hima, kimbia, njoo.

. . . chini . . .
Hupoteza waa lao lote la hatia.

Hupoteza . . .

127 Mwabuduni tu sasa katika Roho. Acha tu moyo wako uwe huru. Sijali wewe ni wa kanisa gani. Moyoni mwako, tu "Asante, Mungu mpendwa."

Na wenye dhambi . . . chini ya gharika hilo,
. . . lao la hatia . . .

128 Sasa ninawatakeni mwinue mkono wenu, ninyi Wakristo, sasa, waaminio, na kuuimba huu pamoja nami.

Tangu kwa imani nilipokiona kijito kile
Kilichosababishwa na majeraha Yako,

Sio kanuni ya imani sasa, kumbukeni.

Upendo wa ukombozi umekuwa ndio wimbo wangu,
Na utakuwa hivyo mpaka nitakapokufa.
Na utakuwa hivyo mpaka nitakapokufa,
Na utakuwa . . . (Huo utakuwa wangu . . .) . . . nitakapokufa;
Ukombozi . . . (Si mwenye kudhihaki, bali upendo wa ukombozi.) . . . umekuwa ndio wimbo wangu,
Na utakuwa hivyo mpaka nitakapokufa.

129 Unamaanisha, Kwake? Semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Na iwe hivyo. *Imani Yangu Inakutegemea Wewe*.

130 Ni wangapi walio wagonjwa na wahitaji, asubuhi ya leo? Baada ya msaada wa kiroho, unahitaji msaada wa kimwili. Inua mkono wako, ndipo tunaweza kukuona. "Mimi ni mhitaji, Ndugu Branham. Ni—niko hapa. Mimi ni mgonjwa. Si—siwezi kupona kamwe. Nimejaribu. Nimeenda kwa daktari. Nimefanya

yote niliyojua kufanya, bali kamwe siwezi kufaulu, inaonekana. Lakini ninaamini ya kwamba Mungu atanipa afya." Unaamini hilo? Hiyo ni ahadi Yake.

131 Sasa, je, umepandwa kandokando ya mito ya Maji? Maji yapi? Yule Kristo aliyepigwa; ambapo, kutoka mwambani kulibubujika maji, yapate kuwaokoa watu kutoka mautini. Kristo alipigwa, na kutoka mwilini Mwake akatoka Roho Mtakatifu, kusudi watu wanaoangamia wasije wakafa bali wawe na Uzima wa Milele. Je, wewe . . . Kuna mambo mengi tofauti.

132 Mungu anaahidi kuponya. "Alijeruhiwa kwa makosa yetu, akachubuliwa kwa uovu wetu; adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake; kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa." Mito, mito ya Maji mamoja, Roho Mtakatifu.

133 "Kunao, kwanza, mitume, manabii, walimu, wainjilisti, wachungaji," mito ya Maji mamoja.

134 "Pana karama mbalimbali. Wengine wameitwa kutabiri. Wengine wameitwa, wamepewa karama ya uponyaji. Wengine wana hekima. Wengine wana maarifa, kwa Roho yeye yule. Wengine wananena kwa lugha. Wengine wanafasiri. Wote kwa Roho yule yule," Wakorintho wa Kwanza 12. Ni kitu gani? Mito, mito ya maji mengi, maji mengi.

135 Mito mingi ya Maji mamoja, Roho Mtakatifu akitoa karama nyingi na baraka kutoka kila mahali. Analeta karama tele, pia, karama za uponyaji, karama za wokovu, karama za Roho Mtakatifu kwa kutenda kazi kanisani mwenu na miongoni mwa watu. Mito! Na furaha kama mto na chemchemi. Ni zuri jinsi gani!

> Imani yangu inakutumainia Wewe,
> Ewe Mwana-kondoo wa Kalvari,
> Mwokozi wa Kiungu;
> Sasa nisikie niombapo,
> Ondolea mbali dhambi zangu zote,
> Loo nijalie tangu leo
> Niwe kabisa . . .

136 Sasa, Bwana, hayo ndiyo maombi yetu. Hatutakuwa na haraka. Hii ni sabato. Hii ndiyo siku ambayo Wewe umeifanya. Inatupasa kukuabudu Wewe siku nzima. "Mchana kutwa na usiku kucha," mshairi alisema, "Malaika wanaendelea kunilinda." Sasa tunahisi ya kwamba Hao wako karibu.

137 Baba Mungu, nimenena jambo kali sana. Bali sikufanya hivyo . . . Uchunguze moyo wangu, Bwana. Kama nilifanya hivyo kwa kijicho, basi nisamehe. Lakini nilifanya hivyo kwa ajili ya upendo kwa tawi Lako, Mzabibu Wako. Ninaomba, Bwana, ya kwamba kukiweko na wengine hapa walioshirikishwa katika madhehebu makuu, kumbuka . . . sijaribu kuwaomba watoke kwayo. Ninawaomba tu wasifungwe na kanuni yao ya imani, bali waje Kwako, wapate kufunguliwa na kulimwa, naye

Roho amwagwe ndani. Ndipo kanisa lao litakuwa kanisa bora zaidi, kanisa la kiroho, ambalo unalijia, lisilo na waa wala kunyanzi, lililooshwa katika Damu ya Mwana-Kondoo. Ulimwengu huu wa kiakili, siku hizi, Baba, umeliondokea hilo kwa mbali. Wanatazamia umati mkubwa na makanisa makuu, kama mzabibu mwitu. Lakini, Bwana, sisi—sisi tunashikilia tunda hilo tamu, tunda hilo la Roho, linaloleta utamu kwa nafsi yetu.

138 Tunaomba sasa kwamba uwabariki watu hawa wagonjwa wanaokuja mbele wakaombewe. Bwana, ninaweza kukuomba mara nyingine tena, je, waweza kulitakasa tawi hili lisilostahili, kwa Damu Yako? Ili kwamba Roho Wako aweze kumwagwa ndani yake, kumwonyesha Mungu aliye hai, kwamba Wewe ni Mungu yeye yule aliyenena na yule mwanamke kisimani. Jalia iwe hivyo, ili watu waweze kupita kuchanganyikiwa, wapate kuona mahali Roho wa Mungu alipo hasa, ni ndani ya moyo wa mwaminio, sio katika kanisa fulani, bali katika moyo wa mwaminio. Lijalie, Baba. Nitakungojea Wewe sasa, upate kujionyesha Mwenyewe, kama ulivyojionyesha katika siku za kale. Kama ulivyojionyesha Mwenyewe kupitia Yesu, Yule aliyekufa tupate kuwa safi, kusudi Roho yule yule aliyekuwa ndani Yake aweze kuja kupitia sisi, akitoa matokeo yale yale. Lijalie, Baba. Kwa kuwa nayakabidhi mambo yote Kwako, katika Jina la kupendeza la Mwana Wako, Yesu. Amina.

> Wala usiniache nikaondoka
> Kutoka Kwako kwenda kando.

139 Vema, Teddy, *Amini Tu*. Sasa ni wangapi humu ndani ambao . . .? Billy alisema alisambaza kadi kadhaa za maombi.

140 Sasa tumekuwa, kanisani, kwa kuwa tumesongamana, tukichukua tu na kuwaomba wote walio wageni miongoni mwetu wasimame, na kuacha Roho Mtakatifu apitie kwenye watu hao na kuwatambua namna hiyo. Tulifanya hivyo, mara nyingi. Sasa, majuma machache yaliyopita, mtu fulani alisema, "Lakini ni vigumu kwa watu kushika hilo. Lakini wanataka mstari wa maombi." Kwa hiyo sisi . . . Ni wangapi wamekuwa hapa wakati Roho Mtakatifu alipitia juu ya umati na kumchukua kila mtu kutoka kwenye umati? Hakika.

141 Sasa, nilimwambia Billy asambaze kadi za maombi, tupate kuwaita, kwa makundi, na kuwaombea, mnaona, kulimalizia.

142 Kwa hiyo basi, na mara baada ya hili, watakuwa na ibada ya ubatizo kwa ajili yenu mnaotaka kubatizwa. Tutawapa mahali, wakati, katika dakika chache tu.

143 Kwanza, tumezungumza juu ya huu. Tumezungumza juu ya Mzabibu huu, urithi huu wa Mungu. Sasa, kama hiyo ni kweli, basi kama kweli sisi ni tawi lililochaguliwa tangu zamani kwenye huo Mzabibu, basi Roho Mtakatifu yule yule hana budi kuja kupitia sisi. Na kama akipitia, atafanya jambo lile lile

alilofanya kupitia Kwake, kwa kuwa Yeye ndiye Mzabibu. Sisi ni matawi. Na kama . . . Uhai ulio katika mzabibu hauna budi kuwa katika tawi, kulifanya tawi liishi. Kama ukizaa tofauti na kile Mzabibu ule ulichozaa, basi ni mzabibu mbaya. Hivyo ndivyo ninavyojaribu kusema. Hauna budi kuwa ni Uhai ule ule.

144 Sasa, ni nani walio na kadi za maombi? Inua mkono wako! . . . ?. . . Vema. Zinaanzia wapi, kutoka moja hadi hamsini, ama moja hadi mia moja? Ama, ni wangapi wajuao? Ka—kadi za maombi ziko mbele . . . Ngojeni. Sasa, ni nani aliye na namba moja? Kuna kadi ya maombi namba moja hapa ndani? Kunayo? Vema, zilianzia wapi, basi, hamsini? [Ndugu fulani anasema, "Moja hadi hamsini."—Mh.] Loo, loo, hapa, moja hadi hamsini. Vema.

Simama papo hapo, unaona, namba moja.

Namba mbili. Namba mbili. Vema, simama papo hapo.

145 Namba tatu, kadi ya maombi namba tatu. Imo jengoni? Wanaweza kusimama? Samahani. Wanazipata, kila mahali. Namba tatu, waweza kuja hapa, mama?

146 Namba nne. Ni nani aliye na kadi ya maombi namba nne? Nenda pale pale, mama. Namba nne, niliiona hiyo? Hiyo ndiyo . . . Ni nani aliye na namba nne? Vema.

Namba tano, namba sita, saba, nane. Nane, namba nane.

147 Tisa. Sasa ngojeni hapa. Namba nane, tisa. Watu wengine wametoka nje, kwa hiyo huenda ikawa, huenda alikuwa mmoja wao. Namba tisa.

148 Namba kumi, namba kumi na moja, namba kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na nne, kumi na tano.

149 Whiu! Nimekosa wanne ama watano. Kwa hiyo tutaifikia. Labda alitoka nje. Kama mtu yeyote akiingia, Ndugu Taylor, angalia uone kama wana kadi za maombi huko. Waingize upesi mstarini, tafadhali. Kama huenda hata walienda hapo nyuma mahali fulani.

150 Sasa nitaomba muwe na uchaji mkamilifu, na muwe tu na uchaji kabisa.

151 Ni wangapi hapa ndani ambao ni wagonjwa wala hawana kadi ya maombi? Mwaweza kuinua mikono yenu na kusema, "Mimi ni mgonjwa na mhitaji wala sina kadi ya maombi." Vema. Sasa angalieni huku na muamini. Vema.

Sasa, Ndugu Teddy, polepole kabisa.

152 Sasa, kama watu hawa hawaingii, tunaweza kuendelea na mstari wa maombi, mahali pengine. Lakini tutangojea, kuwapa nafasi.

153 Sasa, huu hapa wakati ambapo kila kitu ambacho nimesema hakina budi kuthibitishwa kuwa ni kweli ama si kweli. Hivi Biblia haisemi, "Jaribuni mambo yote. Pia lishikilieni sana lililo

jema"? Sasa endapo . . . Yesu, akiwa ndiye Mzabibu wa Mungu, uliojizungusha kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu, alilileteа Kanisa Uzima wa Milele, nasi ndio matawi ya Mzabibu huo. Mnaona?

154 Yeye aliwapanda Israeli katika Palestina. Halikufanikiwa. Wakawa kama . . . Matunda yao yalinyauka kama kuvu mviringo. Yalikua upesi mno, kisha yakatoweka, ikionyesha hayakuwa sawa. Hayakuwa na "Milele."

155 Lakini matunda yaliyomo katika Kristo Yesu yatadumu milele. Hayana budi kudumu. Basi kama Roho Wake, aliyekuwa juu Yake, angali hai leo hii, Yeye si dhehebu la kuvu mviringo. Ni Mungu aliye hai anayetoa Uzima ule ule aliokuwa nao. Mnaamini hilo?

156 Sasa, halitapasuka tu na kusema, "Loo, hayo mambo yalikuwa kwa ajili ya siku nyingine. Loo, ni kitu kama *hiki*." Likifanya hivyo, utang'olewa, asubuhi ya leo.

157 Ni halisi. Ni Uzima halisi. Ni Kristo halisi. Sasa iweni na imani na muamini, msione shaka hata kidogo kwamba Mungu yupo hapa kuwaponya wagonjwa.

158 Sasa, wewe usiye na kadi ya maombi, kama utaomba na kuamini tu kwa moyo wako wote, basi—basi Mungu ataninii, Mungu atakujalia mambo uombayo. Ni wangapi wanaoamini hilo sasa?

159 Sasa nataka kuwaulizeni jambo moja zaidi. Kama Mungu atafanya hivyo . . . Sasa hebu tuone kama kuna mtu yeyote kwenye mstari huu nimjuaye. Hakuna mtu hapo nimjuaye.

160 Naam, Dada Logston. Wewe si ni Dada Logston? Sivyo? [Dada Logston anasema, "Siko mstarini."—Mh.] Loo, huko mstarini. Sa—samahani.

161 Nadhani watu hao wote ni wageni kwangu sasa. Hiyo—hiyo ni kweli? Sijui lolote kuwahusu. Inueni mikono yenu kama hiyo ni kweli. Hapo, kwani hilo lilitukiaje? Kweli hilo lilitukiaje, kwa kushuka tu hapa na kusambaza mstari mzima wa kadi za maombi, mtu yeyote anayezitaka hapa, hata kwa wale labda walio . . . ha—hawako? Kwani hilo lilitukiaje? Mstari mzima pale, hakuna mtu hapa sasa maskanini. Siamini hilo lilipata kutukia hapo awali.

162 Sasa ninyi msio na kadi ya maombi. Kulikuwako na mwanamke ambaye alipitia kwenye umati, wakati mmoja, na kugusa upindo wa vazi Lake, kwa kuwa yeye alisema, "Ninaamini. Sijali yale kuhani asemayo, wala mtu mwingine yeyote. Ninamwamini. Kama ninaweza kuligusa vazi Lake nitaponywa." Mnaijua hadithi hiyo? Naye akaligusa vazi Lake. Ndipo akamgeukia na kumwambia ya kwamba kutokwa kwake na damu kulikuwa kumekoma. Imani yake ilikuwa imemponya. Mnajua hilo kuwa ni Kweli?

163 Vema, Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule asubuhi ya leo. Yuko kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu. Neno Lake, hilo ni matawi Yake. Neno la Mungu limeunganishwa na Kiti cha Enzi cha Mungu kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Mnaamini hilo? Lilileta Uzima, Kristo Yesu. Kupitia Uhai huo, liliingiza matawi, linaleta Uhai ule ule lililo kutoka kwenye Kiti cha Enzi. Hiyo ni kweli? Kisha Yeye anaketi, hali ya mizizi Yake siku hizi, yuko kwenye mkono wa kuume wa Ukuu Mbinguni, kuleta Uhai ule ule kupitia Kanisa Lake. Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Hiyo ni kweli, sivyo? Sasa wewe amini hilo kwa moyo wako wote.

164 Akifanya hivi, ni wangapi wenu ninyi wagonjwa huko nje mtalikubali? Ninyi nyote? Sasa, Teddy . . .

165 Sasa huyu hapa mwanamke amesimama, ambaye ndio kwanza ainue mkono wake kwamba sikumjua. Naye Mungu anajua hilo, nijuavyo mimi, sijawahi kumwona hapo awali.

166 Hata anaweza kuwa ametoka humu mjini. Sijui. Sijui theluthi moja ya watu tena. Watu wapya wamehamia huku. Nilikuwa nikishuka katikati ya mji, ni—nilimjua kila mtu. Sasa, karibu simjui mtu yeyote, maana imeingia tu ndani.

167 Simjui huyu mwanamke. Yeye hanijui. Lakini kama Uhai ule ule uliokuwa katika Mzabibu huo, ambao uliahidi kwamba tawi litaleta mstari ule ule ambao . . . Uzima ule ule ambao huo Mzabibu ulileta. "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Je, hayo ni Maandiko? Yohana Mtakatifu 14:8. Vema.

168 Sasa, kama kazi aliyofanya, alizungumza na yule mwanamke kisimani na kumwambia jambo ambalo lilikuwa ni kitu kilichofichika maishani mwake; kama Roho Mtakatifu yeye yule, asubuhi ya leo, atafanya kazi kupitia humu kanisani, na kunena kupitia kwangu, na kumwambia mwanamke huyu jambo fulani ambalo limemleta hapa, ama jambo fulani ambalo limekuwa maishani mwake, au kitu kingine ambacho anajua sijui chochote juu yake. Maana, kama simjui, vema, si—sijui chochote kumhusu. Amesimama tu hapa.

169 Lakini kama Roho Mtakatifu huyo atalijalia hilo, kutoweza kukosea. Hili hapa Neno la Mungu, lilililiahidi. Sote wawili tuko hapa, tukisema, sote wawili, "Kamwe hatufahamiani, kamwe hatujawahi kuonana." Ikiwa Roho Mtakatifu atafunua hilo, basi, Uhai ule ule uliokuwa katika tawi hilo ungali hai, ama katika ule Mzabibu, hasa, ukipigapiga kupitia kwenye hilo tawi. Bwana Mungu na alijalie.

170 Sasa, katika Jina la Yesu Kristo, ninachukua kila roho humu ndani chini ya mamlaka yangu, kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Sasa, sasa iweni tu na kicho kabisa, kila mtu.

171 Tunakutana kwa mara yetu ya kwanza, mwanamume na mwanamke, ni kitu kama ilivyokuwa katika Maandiko. Mungu

anaruhusu hili, pengine, kusudi watu, kwenye Siku ya Hukumu, wajue, wasiwe na udhuru. Kama mtu yeyote angeondoka asubuhi ya leo, bila kupandwa ndani ya Kristo, bila kujua wema Wake na rehema Zake; bila hiyo hapo, angekuwa na nafasi ndogo sana, ningewazia, kwenye Siku ya Hukumu. Wakati Neno limehubiriwa, ndipo iwapo Roho Yake . . .

172 Mnaona, kuna jambo moja, kuhubiri jambo fulani. Kama Yeye ni Mungu wa kihistoria, basi hilo ni lile tu alilofanya katika historia. Lakini kama Yeye kweli ni Mzabibu, nasi ni matawi, basi tawi ni sehemu vivyo hivyo. Uhai ulio ndani ya Mzabibu unadundadunda moja kwa moja kupitia kwenye tawi, mnaona, kwa hiyo itabidi uzae kitu kile kile. Aliahidi hilo. "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya."

173 Sasa, kama wewe ni mgonjwa, na, hilo—hilo sijui. Lakini iwapo wewe ni mgonjwa, singeweza kukuponya, kwa maana Yeye tayari amefanya hivyo.

174 Lakini huenda ikawa kwamba Uwepo Wake hapa ungekufanya uelewe kikamilifu ya kwamba Yeye yuko hapa. Basi hilo lingeinua imani yako kulikubali. Unaona? Hivyo ndivyo lingefanya kwa kusanyiko. Kile lingemfanyia mwanamke huyu, lingemfanyia kila mmoja wenu. Sasa aminini tu hilo.

175 Sababu, "Alijeruhiwa kwa makosa yetu. Kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa." Tuliponywa. Zamani za kale, miaka elfu mbili iliyopita, wokovu na uponyaji ulikuja wakati huo.

176 Sasa unasema, "Unazungumzia nini, Ndugu Branham?" Ninaona kile Roho Mtakatifu atakachosema. Simjui.

177 Basi mahali pagumu zaidi nilipopata kufanyia mkutano, ni papa hapa. Maana, hivyo ndivyo Kristo alivyosema, "Nabii katika nchi yake, miongoni mwa watu wake." Mnaliona? "Aliingia kwa walio Wake, na mambo mengi hangeweza kufanya." Akaondoka. Sasa, si kwa sababu kikundi hiki kidogo hapa. Hilo silo. Kanisa langu, wananipenda na kuniamini. Lakini ni elementi ya nje. Nalo Neno la Mungu lilisema. Linasema hivyo.

178 Lakini ni—ninasimama kwa muda kidogo tu, kuona kama Roho wa Mungu atanipaka mafuta nipate kujua. Sasa, yeye ni roho na yeye ni mwili. Siku moja hiyo roho itaondoka, ndipo basi mwili utaoza. Roho inakwenda kwa Mungu aliyeitoa. Hapa kuna roho, pia, imesimama hapa, lakini imewakilishwa katika mwili wa nyama. Sasa kama roho hizi zimeunganishwa kwenye Mzabibu huo, utazaa . . .

179 Ilikuwa ni nini? Roho ilipokuja mbele za Yesu, iliyokuwa na kasoro fulani, huyo Roho aliyekuwa ndani Yake alilifunua. Mnaona? Naye mwanamke huyo, wakati Yeye alipoifunua, aliikubali, na kusema, "Hapana shaka Wewe ni Masihi. Tunajua ya kwamba atakapokuja, atatuambia mambo haya."

180 Petro, wakati alipokuja, loo, kidogo alishangaa yale Andrea aliyokuwa akizugumzia. Akasema, "Yeye ni Masihi." Basi alipofika Kwake, Yeye alisema, "Jina lako ni Simoni. Wewe ni mwana wa Yona." Hilo lilimtosha. Unaona? Alijua hakujua yeye ni nani.

181 Lakini Yeye anajua wewe ni nani. Mimi sijui wewe ni nani, lakini Yeye anakujua. Sijui chochote kukuhusu wewe, lakini Yeye anajua.

Sasa, Huyu hapa. Sasa Roho wa Mungu yuko hapa madhabahuni.

182 Sasa, basi, Wewe ulijua jambo fulani lilitukia. Uko hapa kwa sababu ya ugonjwa wa neva. Hiyo ni kweli. Una yabisi kavu, pia. Hiyo ni kweli. [Dada huyo anasema, "Ndivyo ilivyo."—Mh.] Unaamini? Sijawahi kumwona huyu mwanamke maishani mwangu.

183 Sasa, hilo si ni tamu, hiyo kweli. . . Ninajua huna budi kuihisi. Ninaitazama. Unaona? Ni kama tu mvuto mtamu.

184 Hapana, naona mwanamume akija hapa juu. Ni ndugu yako. Umekuwa ukimwombea sana. Ninamwona mtu mdogo zaidi, mdogo zaidi. Hapana shaka ni mhudumu. Ni mwanao. Ana shida ya kiroho. Umetoka mbali sana, kufika hapa. Unatoka Kusini, ukija huku. Unatoka Tennessee. Wewe ni Bibi Tabor. Rudi huko. Umepata haja yako. Mungu amekupa. Kama . . .

185 Sasa, kamwe sikumgusa mwanamke huyo. Roho Mtakatifu alifanya hivyo. Sasa, hiyo ni vivyo hivyo. Je, hivyo ndivyo ilivyotukia katika Biblia? Mwanamke huyo alisema, "Hapana shaka Wewe ni Masihi." Sasa, hiyo haimaanishi *mimi* ni Masihi. Hiyo inamaanisha kwamba Roho wa Masihi yuko hapa. Sisi ni wanaume tu na wanawake. Ni Roho wa Masihi.

186 Sasa, wewe upokee, ung'olewe, kutoka katika kutokuamini huko kwa kale, ukapandwe kando Yake, unaona, sasa. Inuka na useme, "Bwana Yesu, Wewe ukiwa ni Mwana wa Mungu, Kuhani Mkuu. Ndugu Branham ndio kwanza aseme umeketi katika Ukuu Juu. Ulichaguliwa tangu zamani kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ulichinjwa, upate kuleta matokeo haya; ili, mimi, mwaminio nusu, nikijaribu kuamini, nipate kufanywa kuamini kikamilifu. Jalia niguse vazi Lako. Acha yeye aseme nami." Wewe ambaye . . .

187 Ninyi katika kusanyiko, semeni jambo lile lile. "Kwa maana kama Wewe ni yule yule jana, leo, na hata milele, Wewe—Wewe—Wewe niruhusu nikuguse kwa imani yangu, nikiweka kando mawazo yote ya kutokuamini. Acha nikuguse Wewe."

188 Ninaamini uliinua mkono wako, pia, kwamba tulikuwa hatufahamiani. [Dada huyo anasema "Niliinua."—Mh.] Vema. Sasa, kama Bwana Yesu anaweza kunifunulia, shi—shida yako, au kitu fulani kwa njia fulani, ungeamini hilo, ya kwamba

Kamba hii okozi, ya kwamba Kanisa kweli limepandwa katika Mungu. Yesu alisema, "Siku hiyo, mtajua ya kuwa Mimi niko ndani ya Baba, Baba yu ndani Yangu; na Mimi ndani yenu, nanyi ndani Yangu." Mnaona? Ni ule Uzima wa Mungu unaotiririka moja kwa moja kupitia Jina la Yesu Kristo, moja kwa moja kuingia Kanisani, unaona, hutufanya mmoja. Sisi ni matawi. Sisi ni wawakilishi Wake.

189 Kama unaamini hilo, hiyo shida ya mguu itakuacha. Je, utaamini? [Dada huyo anasema, "Naamini. Naamini."—Mh.] Vema. Unaweza kuupata. Naye mume wako pale angeponywa, pia. Unaamini ataponywa, hiyo ngiri? ["Naam."] Na wewe, bwana, unaamini kwamba utapona? [Ndugu huyo anasema, "Amina."] Uh-huh. Unaamini? Una binti, pia. Ana roho ya tatizo fulani la kiroho. Umetoka Kaskazini, ukija huku. Umeshuka kupitia barabara kuu. Unatoka Austin. Jina lako ni Bibi White. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. ["Loo!"] Rudi na uamini sasa, na uponywe, kisha upate afya. Mungu akupe shauku ya moyo wako.

"Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana."

190 Uhai wa Uzima wa Kristo, katika tawi. Hilo tawi si Maskani ya Branham. Tawi si William Branham. Tawi ni mtu yeyote atakayeng'olewa kutoka katika kutokuamini kwako, na kupandwa ndani Yake.

191 Ninaamini uliinua mkono wako kwamba, pia, tulikuwa hatufahamiani. Sikujui wewe. Mungu anakujua. Huko hapa kwa ajili yako mwenyewe. Ni kwa ajili ya mtoto. Ninaiona ile Nuru ikining'inia juu ya huyo mtoto. Ikiwa Mungu atanifunulia tatizo la mtoto wako, je, utaniamini mimi kuwa ni nabii Wake, na kuamini kwamba nakwambia ukweli? Ungeamini. Huyo mtoto ana ugonjwa wa moyo. Ni kitu kama vali, daktari alisema. Amechunguzwa. Anataka kumpeleka kliniki mara moja. Hiyo ni kweli. Unatoka hapa Jeffersonville, hapa mtaani, Mtaa wa Fulton. Lakini hiyo ni kweli. Na jina lako ni Bibi Burkhart, Irene Burkhart. Rudi huko, na uamini kwa ajili ya huyo mtoto mchanga, atapona.

192 "Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana." Ukiamini tu!

193 Mwanamke huyu aliyeketi hapa akiwa na shida hiyo ya mishipa. Naam. Sahau hilo. Unaenda nyumbani, uwe mzima sasa.

"Kama unaweza kuamini!"

194 Umeinua mkono wako juu namna *hii*, una shida ya mgongo. Unaamini Mungu atakuponya? Unaamini, unaukubali? Basi nenda nyumbani na uwe mzima. Yesu Kristo akuponya.

195 Yako ni figo. Kwa hiyo, endelea, umepata wako, pia, bwana. Mungu akubariki.

Mwamini Mungu. Usitie shaka.

196 Mwanamke mweusi. Kunao wawili. Moja kwa moja kule nyuma kabisa. Uvimbe kooni, ndani ya koo. Amini kwa moyo wako wote. Unaamini hilo, mama? Kitu kama kofia ndogo, juu pale. Unaamini? Inua mkono wako. Vema. Nenda nyumbani; utakuacha.

197 Kunaye msichana mdogo wa umri kuliko huyu. Sikujui. Mungu anakujua. Unaamini Yeye anaweza kukuponya? [Dada huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Vema, rudi New Albany, Bi Pearl Allen, na ukaponywe. Yesu Kristo alikuponya. Nenda, ukiamini, unaweza kupona.

198 Mwaminini Mungu. Mnaamini kwa moyo wenu wote? Sasa, si. . . Loo, kuna kila kitu kinachotukia, juu ya. . . Ikiwa tu unaweza kuamini, rafiki!

199 U hali gani, bwana? Unamwamini Yesu Kristo Mwana wa Mungu? Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? [Ndugu huyo anasema, "Ninaamini."—Mh.] Unaamini kwamba yale ningekwambia. Ungejua kama ni kweli au si kweli. Unaamini yale niliyohubiri, asubuhi ya leo, ni Kweli? ["Naam."] Unaamini. Uko hapa kwa ajili ya jambo zuri. Uko hapa kuondolea mbali tabia fulani, hiyo ni, uvutaji sigara. Ninakuona ukiitazama, na kukihukumu kitu hicho, na kukiweka mbali nawe. Hiyo ni kweli. Usininii. . . kama wewe. . . Sikiliza. Unataka maombi kwa ajili ya mke wako. Kidogo ana kitu kama vipindi vya kizunguzungu. Bw. Carlock, rudi Owensboro, Kentucky, ulikotoka. Usiguse nyingine. Yesu Kristo anakufanya mzima. Nenda, katika Jina la Bwana, ukaponywe.

Mnaamini?

200 Sasa tazameni. Mtu huyu anayekuja hapa, weka tu mkono wako juu ya wangu, bwana, hapa. Shida yako ya mgongo imekwisha. Rudi tu kupitia pale, ukimshukuru Mungu. Amina.

201 Unataka kwenda kula chakula chako cha kutwa? Shida ya tumbo itakuacha kama ukiamini. Unaamini? Nenda zako. Msifu Mungu tu, na kusema, "Asante, Bwana."

202 Ni wangapi wanaamini kwa moyo wenu wote?

203 Mungu akubariki. Vivyo hivyo, pia, unaweza kwenda na kumsifu Bwana. Useme, "Asante, Bwana."

204 Una shida ambayo watu wengi hapa nje wanayo. Ni wasiwasi, huufanya moyo wako ufanye makelele, na ugonjwa wa moyo. Ikiwa unaamini kwa moyo wako wote!

205 Huko nje, ni wangapi walio na moyo wenye wasiwasi na kadhalika? Sasa inueni mikono yenu namna *hiyo*. Angalia hapa. Ungewezaje kuiita kamwe? Unaona?

206 Unaamini kwa moyo wako wote? Unaamini, pia? Vema. Nenda ukaponywe katika Jina la Yesu Kristo. Usiwe na shaka hata kidogo, lakini amini yale uliyoambiwa kwamba ni Kweli. Amini kwamba umeponywa. Uliyoomba yatakuwa yako.

207 Ninyi wengine fanyeni vivyo hivyo. Ni wangapi wengine kati yenu hapa nje mlio nayo? Vema, bwana. Je, ni wangapi huko nje wanaomhitaji Mungu? Inueni mikono yenu. Na kusema . . .

208 Tazama. Shikeni hili. Siwezi kumponya mtu yeyote. Mimi ni mwanadamu. Kama Kristo alikuwa amesimama hapa, asingeweza kumponya yeyote wenu. Ameandaa mpango, na mpango huo ni wewe uamini ya kwamba alikufa kwa ajili yako, unaweza kuponywa kwa huo. Hiyo ndiyo njia pekee. Ni uponyaji wa imani. Imani! Amini kwamba Kristo amelipa deni kwa ajili yako. Ni wangapi wanaelewa hilo sasa? Vema. Ni wangapi wanaokubali hilo? Vema.

209 Tunapoomba, wekeaneni mikono ninyi kwa ninyi. Wekeaneni mikono ninyi kwa ninyi, kila mmoja aombe.

210 Sasa unaweza kwenda kwenye kiti chako, dada. Mungu akubariki sasa. Uwe mzima! . . . ? . . . Ndiyo. Hiyo ni kweli. Ni ugonjwa wa wasiwasi, lakini uta—utakuacha. Shuka kupitia pale sasa, uone kama hiyo . . . Umeanza kujisikia tofauti, sivyo? Unaona? Hakika. Uliponywa, ukisimama papa hapa. Mnaona jinsi alivyotoka kwenye hicho kipandio bila hayo? Unaona? Na sasa uko sawa. Sasa unaweza kwenda nyumbani, uwe mzima. Bwana akubariki.

211 Sasa huku mmewekeana mikono. Mnaona, hatuna muda mwingi, ni karibu adhuhuri. Nao wangali wana ibada ya ubatizo, bado.

212 Hakika, hakika, watu, ule Uzima mkuu wa Mungu, yule Roho Mtakatifu mkuu Ambaye bila kosa alionyesha ya kwamba Yeye yuko, anaonyesha ya kwamba Uhai huo unaotoka kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu unapigapiga kwenye yale matawi, kuonyesha Uzima. Hivi hamuamini hilo? Basi, la, kamwe sikumponya hata mmoja wa watu hawa waliokuja hapa. Imani yao iliwaponya kwa sababu waliambiwa kitu ambacho ni kweli. Kama ungekuwa hapa, Yeye angefanya vivyo hivyo.

213 Sasa kwenu huko nje, Yeye anawafunulia kile mnachohitaji. Sasa tunapoomba, sote pamoja, ombeni, aminini kila neno kuwa ni kweli, muone kitakachotukia. Mtaponywa. Sasa wewe mwombee mtu huyo. Usijiombee mwenyewe. Mwombee mtu ambaye umeweka mikono yako juu yake. Acha mtu huyo akuombee. Kuombeana. Biblia inasema hivi sasa.

214 Biblia ile ile iliyosema, "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya," ilisema hivi, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Sasa, Mungu yule aliyefanya ahadi moja, na kuitimiza, ikiwa umepandwa humo, kandokando ya mito ya Maji, huleta kila Uwepo wa Kiungu wa Mungu, kila ahadi, moja kwa moja kwenye uhusiano wako. Wewe ni mti uliopandwa kandokando ya mito ya Maji mamoja. Maji hayo mamoja ni Kristo, Roho Wake Mtakatifu. Kuna uponyaji. Kuna wokovu. Kuna furaha.

Kuna uvumilivu, upole, unyenyekevu, uvumilivu. Kila aina ya karama zimewekwa moja kwa moja katika Jina hilo moja la thamani. “Lolote mtakalomwomba Baba katika Jina Langu, hilo nitafanya.”

215 Sasa wewe omba katika Jina la Yesu, kwa ajili ya mtu uliyemwekea mikono yako. Nitawaombea wote, ninyi nyote. Hebu Roho Mtakatifu, aliyepo sasa, amponye kila mtu.

216 Bwana, tungeomba kwamba fadhili Zako ziendelee kuwa pamoja nasi. Kila mmoja anaomba kwa njia yake mwenyewe. Wamemwona Roho wa Mungu aliye hai akifanywa kuwa halisi tu kama alivyokuwa huko Galilaya. Kama vile tu alivyokuwa wakati Petro alipofika pale kando ya pwani ya Galilaya, naye Yesu akamwambia kuwa yeye alikuwa ni nani. Na halisi tu kama ilivyokuwa wakati Nathanaeli alipokuja, Naye akamwambia mahali alipokuwa siku iliyotangulia. Halisi tu kama ilivyokuwa kwenye lango la Samaria, ama pale kisimani. Hakika watu wangeweza kusema, “Huyu ni Roho wa Mungu aliye hai.”

217 Bwana, tupe imani na akili timamu, na Uwepo wa Roho Mtakatifu, ili kila mmoja, akiomba, aweze kumwombea mwenzake, maombi ya imani. Ninawaombea sasa, Bwana, wale ambao wameweka mikono yao juu ya mtu fulani, ya kwamba utawapa imani isiyobadilika, sasa hivi kwa ajili ya mtu huyo. Na, bila shaka, hiyo itawarudia. Loo, jalia iwe! Bwana Mungu, na iwe hivyo. Tunaweza kuwaleta, mmoja mmoja, kupitia jukwaani, pamoja na matokeo yale yale; lakini bado itahitaji imani, imani katika mtu binafsi, kumwamini Mungu. Nayo imeandikwa, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.”

218 Ee Bwana, timiza ahadi Yako asubuhi ya leo, kwa kila mwaminio. Na jalia Roho Mtakatifu sasa hivi aingie katika miili ya wagonjwa hawa, na kuondoa maradhi yote na magonjwa. Na kuwe na thibitisho kubwa sana hata mioyo ya watu hao itaruka kwa furaha, wakiamini kwamba Mungu amewaponya. Jalia waondoke kwenye maskani hii, wakiimba na kushangilia, na kuamini ya kwamba Mungu amewaponya. Jalia warudi kwenye tarehe nyingine, wenye furaha, wakishangilia, wakishuhudia, kama vile mamia wangeweza kushuhudia leo kote ulimwenguni, juu ya Nguvu Zako za uponyaji. Maombi haya tunayasema juu ya watu hawa, tukiomba iwe hivyo, katika Jina la Yesu Kristo Mwana wa Mungu. Nuru ya Mungu na iangaze na kuwaponya wote. Amina.

> Ninaweza, nitaamini, kweli ninaamini;
> Ninaweza, nitaamini, kweli ninaamini;
> Ninaweza, nitaamini, kweli ninaamini
> Ya kwamba Yesu ananiponya sasa.

Je, unaamini? Inua mkono wako.

Ninaweza, nitaamini, kweli ninaamini;
Ninaweza, nitaamini, kweli ninaamini;
Ninaweza, nitaamini, kweli ninaamini
Ya kwamba Yesu ananiponya sasa.

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . amini hilo.

219 Ningetembelea nyumba za watu, nao wangepika chakula kizuri cha kutwa. Inawabidi kunichemshia kikombe cha maji ya moto, na kuniketisha karibu na uji kidogo wa shayiri; hao wakiwa na kila namna ya vitu vizuri mezani. Siku moja nilimwambia Bwana, "Naamini. Naamini." Loo, jamani! Nilitembea barabarani huku tumbo likiwa na chakula cha kwanza nilichotia kinywani, nikiimba:

Ninaweza, nitaamini, kweli ninaamini;

Kingejaribu kutoka; ningekirudisha ndani.

Ninaweza, nitaamini, kweli ninaamini;
Ninaweza, nitaamini, kweli ninaamini
Ya kwamba Yesu ananiponya sasa.

220 Naam. Hiyo imekuwa miaka ishirini na mitano iliyopita. Amekuwa halisi kwangu tangu wakati huo. Ninashukuru sana kwa ajili ya hilo. Na iwe vivyo hivyo kwenu. Mungu awabariki.

221 Sasa watakuwa na ibada ya ubatizo, katika dakika chache tu, naamini; ndiyo, hiyo ni kusema, kama kuna wengine hapa wa kubatizwa katika Jina la Bwana Yesu Kristo. Ikiwa kuna watu kama hao, kusudi tujue kama tuliachilie kusanyiko au—au tuwashikilie kidogo tu, mwaweza kuinua mikono yenu ikiwa mtu fulani atabatizwa katika Jina la Bwana Yesu? Moja, mbili, tatu, nne. Vema. Naomba wanawake waende upande huu *hapa*, nao wanaume *huku*, kwa ajili ya maandalizi, tafadhalini. Wakati tukiimba mara nyingine tena, *Ni*- . . .

*Kupanda Mzabibu Na Mahali Pa Kuupandia* SWA59-0920
(Planting The Vine And Where To Plant It)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumapili asubuhi, tarehe 20 Septemba, 1959, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:



VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org